

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA



**HOTUBA YA MHESHIMIWA PROF.PALAMAGAMBA JOHN
KABUDI, WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA WAKATI WA
UFUNGUZI WA MAADHIMISHO YA WIKI YA MSAADA WA
KISHERIA KITAIFA**

TAREHE 26 NOVEMBA, 2018 MOROGORO

Mheshimiwa Dkt. Kebwe Steven Kebwe, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro,
Prof. Sifuni E. Mchome, Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria,
Ndugu Amon A. Mpanju, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na sheria,
Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro,
Wakuu wa Wilaya mliopo hapa,
Waheshimiwa Wabunge,
Bibi Felistas Mushi, Msajili Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria Nchini,
Waheshimiwa Mahakimu Mawakili wa Serikali,
Mawakili wa Kujitegemea,
Viongozi na Watumishi wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali mliopo,
Wadau wa Maendeleo Mliopo hapa,
Wawakilishi wa Mashirika Wahisani,
Viongozi na Wakuu wa Mashirika na Taasisi zinazotoa Msaada wa Sheria,
Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria mliopo hapa,
Wasaidizi wa Kisheria,

**Waandishi wa habari,
Mabibi na Mabwana.**

Habari za Asubuhi

Kwa namna ya kipekee sana naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na hata kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo.

Kupitia kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria niipongeze Wizara kwa kuandaa na kuratibu maandalizi ya maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa msaada wa kisheria nchini. Lakini kwa kipekee niwashukuru kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa maadhimisho haya.

Vilevile napenda kuwashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Morogoro na viunga vyake kwa kujitokeza kwa wingi katika maadhimisho haya kwa lengo la kutusikiliza na hatimaye kupokea huduma mbalimbali kuhusu Msaada wa Kisheria zilizoandaliwa kwa ajili yenu. Kama mjuavyo shughuli ni watu na watu wenyewe ndiyo ninyi. **Hivyo Karibuni sana.**

Aidha, napenda kuwashukuru sana wadau na mashirika mbalimbali yaliyoshiriki na kufanikisha maadhimisho haya. Natambua ushiriki wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, (TAMISEMI), Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Wizara ya Fedha na Mipango, Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (LST), Mashirika ya Kimataifa na Wadau wa Maendeleo kama UN Resident Coordinator's Office, UNDP, UNICEF, UN WOMEN, UNFPA, UNHCR, DENMARK-DANIDA, UK-DFID, US- USAID, IRELAND-IRISH AID, SWEDEN -SIDA, FINLAND, CANADA –CIDA, NORWAY –NORAD, Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Asasi za Kiraia kama, Mtandao wa Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria Tanzania (TANLAP), ENVIROCARE, na Mashirika yote ambayo yaliwakilishwa katika maandalizi ya shughuli na Mtandao wa Watoa Huduma za Kisheria. Ni vigumu kutaja kila mmoja lakini nachukua nafasi hii kuzitambua taasisisi na wadau wote waalioshirikiana na Wizara, natoa shukrani zangu za dhati kwa kila mmoja kwa nafasi yake ya ushiriki.

Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana

Maadhimisho haya yanafanyika ikiwa ni utekelezaji wa Ibara ya 13(1), (6) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) na Sheria ya Msaada wa Kisheria, Na.1 ya mwaka 2017 na mikataba mbalimbali ya kimataifa juu ya haki za binadamu ambayo Tanzania imeridhia.

Maadhimisho haya hufanyika kila mwaka na mwaka huu yanafanyika kuanzia tarehe 26 hadi tarehe 30 Novemba, 2018. Mawakili, Wanasheria, Watoa huduma ya msaada wa kisheria na Wasaidizi wa Kisheria hutumia muda huu kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi, hii husaidia kutambua haki zao za kisheria kwa maswala ya kisheria wanayokutana nayo katika maisha yao ya kila siku.

Pamoja na mambo mengine maadhimisho haya yanalenga kuwajengea uelewa wananchi wote juu ya Sheria ya Msaada wa Kisheria na kanuni zake. Maadhimisho ya mwaka huu yanaadhimishwa katika Mikoa Mitano. Hivi tunavyoendelea na uzinduzi huu hapa Morogoro, maadhimisho kama haya yanaendelea katika Mikoa ya Singida, Tabora, Kigoma na Kagera. Kauli mbiu ya maadhimisho haya ni;

***“Huduma ya Msaada wa kisheria iwakumbuke wakina
mama na watoto”***

Kauli mbiu ya mwaka huu imechaguliwa kwa kutambua kuwa wanawake na watoto ni moja ya kundi ambalo linakumbana na changamoto mbalimbali katika jamii. Changamoto hizo kwa kiasi kikubwa huhitaji kusaidiwa kisheria. kundi kubwa linaloathirika na migogoro mbalimbali kama migogoro ya ardhi, ajira, ndoa, mirathi na migogoro mingine ni wanawake na watoto na pia kumekuwa na unyanyasaji wa wanawake na watoto ambao umeigharimu jamii na Taifa kwa ujumla.

Kwa bahati kundi hili limekuwa kikipata vikwazo vya kupata huduma za kisheria kwa sababu ya gharama kubwa au kutofikiwa na huduma hizi kwa urahisi. Kwa msingi huo kupitia huduma za msaada wa kisheria zinazotolewa na Serikali na taasisi zinazotoa huduma ya msaada wa kisheria kundi la wanawake na watoto wanaweza wakasaidiwa kwa haraka.

Mwaka huu tunasisitiza kuwa huduma ya msaada wa kisheria iwakumbuke wanawake na watoto. Serikali kwa kuzingatia misingi ya kikatiba Serikali iliona ni vyema kuweka mfumo madhubuti wa kisheria wa kusimamia na kuratibu

masuala yote ya kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi wenye uwezo wa chini katika kutambua na kutatua masuala yanayowasibu pindi migogoro inapotokea na kuhitaji utatuzi wa kisheria, hili linaenda sambamba kwa kugusa makundi ya wanawake na watoto ambao ndio waathirika wakubwa wa migogoro hiyo.

Hapa nchini Ili kupunguza migogoro hiyo, Serikali imeendelea kutekeleza mikataba ya Kimataifa kuhusiana na haki za wanawake na watoto. Mikataba iliyoridhiwa ni; Mkataba wa kuondoa aina zote za unyanyasaji kwa wanawake, uliosainiwa na Tanzania mwaka 1980 (CEDAW) na Mkataba wa Afrika kuhusiana na Haki na Maslahi ya Mtoto uliosainiwa mwaka,1990. Aidha, ulinzi na ustawi wa wanawake na watoto umeakisiwa kwenye ajenda 2030 ya malengo ya maendeleo endelevu yenye nia ya kudhibiti unyanyasaji dhidi ya wanawake na watoto duniani.

Tunatambua kuwa maendeleo endelevu hayawezi kuja bila kuwepo amani na ulinzi imara, haya yote huja kwa kuweka mifumo madhubuti ya kisheria kwa kuheshimu haki za binadamu na kuwepo kwa mifumo imara ya upatikanaji wa haki ambayo itaweka misingi imara ya kisheria na

utawala bora katika ngazi zote kwa uwazi na kuwa na mifumo thabiti yenye kuleta ufanisi.

Serikali yetu kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitunga **Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009**. Pamoja na mambo mengine sheria hii iliweka mifumo thabiti ya utaoji haki kwa mtoto. vilevile **Kanuni za Mahakama za Watoto Na. 182 za Mwaka 2016** zimeweka mfumo na utaratibu sawa wa uendeshaji wa Mahakama za watoto Tanzania Bara na kuhakikisha haki za watoto zinalindwa kwa mujibu wa sheria. Ili kuhakikisha utekelezaji Mheshimwa Jaji Mkuu kwa mujibu wa sheria kwa amezitambua Mahakama za mwanzo 130 kuwa Mahakama za Watoto na kufanya Mahakama hizo kwa sasa kufikia 131 nchini.

Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Msaada wa kisheria ni suala muhimu sana la kuzingatiwa kwa watu wasio na uwezo na wenye haki ya kupata ushauri wa kisheria. Watu wasio na uwezo wanasisitizwa kupata huduma ya msaada wa kisheria kupitia taasisi mbalimbali zilizopo na ambazo zimesajiliwa na kutambulika kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Msaada wa Kisheria Na. 1 ya 2017. Kwa kutambua umuhimu wa kusogeza huduma hii karibu zaidi kwa wananchi, Sheria

imeweka na kutambua kada ya Msajili wa Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria kwa ngazi ya Kitaifa kwa kusaidiana na Wasajili Wasaidizi katika ngazi za Mikoa na Wilaya walioteuliwa kwa **Tangazo la Serikali Na. 215 la tarehe 18/5/2018**, ambao watakua na jukumu la kupokea na kusajili maombi ya Wasaidizi wa Kisheria na Watoa huduma za Msaada wa Kisheria katika maeneo husika. Watoa huduma wa msaada wa Kisheria na Wasaidizi wa Kisheria wanaratibiwa na kusimamiwa na Ofisi ya Msajili, ambayo pamoja na mambo mengine, imepewa jukumu la kuwasajili na kutatua migogoro baina yao wenyewe au na wateja wao.

Pamoja na masuala muhimu ambayo nimeshazungumzia katika Sheria hii; suala la upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria katika mfumo wa haki jina pia ni jambo jipya ambalo tunapaswa kujivunia. Sheria hii inavitaka vyombo husika kuweka mazingira wezeshi kwa waliopo viziuzini kupata huduma ya msaada wa kisheria. Sheria inatoa fursa ya kupata msaada wa kisheria kuanzia unapofikishwa Kituo cha Polisi hadi Magereza.

Katika kutekeleza upatikanaji wa haki kwa wanawake na watoto Sheria ya Msaada wa Kisheria imetambua na

kuainisha utaratibu wa kusajili watoa huduma wa msaada wa kisheria chini ya sehemu ya Tatu na Nne ya Sheria ya Msaada wa Kisheria. Kwa kufanya hivyo huduma ya msaada wa kisheria itarahisishwa kwa kuwawezesha Watoa huduma ya msaada wa kisheria na Wasaidizi wa kisheria kuwafikia wananchi kwa urahisi.

Aidha, moja ya sifa za kipekee ya sheria hii ni kuweza kutanua wigo wa huduma ya msaada wa kisheria kutoka kwenye wigo wa awali wa **Sheria ya Msaada wa Kisheria (mwendo wa makosa ya jinai), Sura ya 21** kwa kuruhusu huduma ya msaada wa kisheria kwenye mashauri ya madai ikizingatiwa kuwa wanawake na watoto ni wahanga wa unyanyaswaji wa migogoro ya ardhi na ndoa.

Vile vile, sheria imeenda mbali zaidi kwa kulinda maslahi ya watoto walio katika vizuizi, chini ya kifungu cha 35, Sheria imeweka ulazima kwa mamlaka inayomshikilia mtoto kuhakikisha anapata huduma ya msaada wa kisheria haraka iwezekanavyo.

Ni rai yangu kuwa wananchi mtatumia fursa hii mliyopewa na Sheria kupata msaada wa kisheria kupitia Serikali na Taasisi zinazotoa msaada wa kisheria ambazo zimejitolea kutoa huduma hiyo. Ushauri wa kisheria

utakaotolewa utawawezesha wananchi kuzitambua haki zao na kuifahamu sheria na taratibu za kimahakama au kwa kuwasuluhisha katika masuala ambayo yatakuwa hayana umuhimu wa kufika Makahamani. Kwa kufanya hivi itapunguza muda mwingi unaotumika kuhudhuria Mahakamani, kuondoa migogoro katika jamii na kujenga jamii yenye amani, mshikamano na maendeleo endelevu.

Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;

Leo tunazindua wiki muhimu sana kwa wananchi kujipatia huduma hii ambayo itatolewa kwa wiki nzima katika viwanja hivi na katika maeneo ya vizuizi kama polisi na magereza. Hivyo, sitaki nitumie muda mwingi zaidi kwa hotuba, bali nataka huduma ya msaada wa kisheria ianze kutolewa kwa wananchi wenye uhitaji sasa.

Kwa mara nyingine tena, nitoe shukrani za dhati kwa washirika wetu wa maendeleo ambao wamekuwa nasi bega kwa bega katika kuhakikisha shughuli hii inafanikiwa. Naomba niwahakikishie kuwa Serikali yetu ya Awamu ya Tano chini ya uongozi imara wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika katika kuwafikishia wananchi huduma hii. Nizipongeze

taasisi zinazotoa huduma ya msaada wa kisheria nchini kwa kazi kubwa mnayoifanya kuwahudumua wananchi, Serikali inatambua na kuthamini sana mchango wenu katika kuhakikisha kuwa wanachi wanapata haki zao. Niwahakikishie utayari wa Wizara na Serikali kuendelea kushirikiana nanyo katika masuala mbalimbali yanayohusu huduma ya msaada wa kisheria.

Serikali inawahakikishia wananchi wote kuwa, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria itaendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa kutenga wiki moja kwa kila mwaka ili kuwasililiza wananchi ambao kwa upande mmoja wameshindwa kupata huduma ya msaada wa kisheria lakini pia kutumia wiki hiyo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kusaidia kutatua migogoro ambayo imekuwa ikijitokeza kwa wananchi.

Baada ya kusema hayo, natagaza rasmi kuwa maadhimisho haya ya Wiki ya Msaada wa Kisheria nchini kwa mwaka 2018 yamefunguliwa rasmi. Karibuni sana tupate huduma ya Msaada wa Kisheria inayotolewa bure kwa wale wote wasio na uwezo wa kumudu gharama za kupata huduma hii.

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA.